ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Jimbo la Mahonda
2.	Mhe.	Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
3.	Mhe.	Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
4.	Mhe.	Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
5.	Mhe.	Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
6.	Mhe.	Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
7.	Mhe.	Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
8.	Mhe.	Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
9	Mhe.	Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
10.	Mhe.	Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
11.	Mhe.	Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
12.	Mhe.	Chum Kombo Khamis	-	Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	Jimbo la Tumbatu
14	Mhe.	Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
15.	Mhe.	Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
16	Mhe.	Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
17.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	Jimbo la Makunduchi
18.	Mhe.	Harusi Said Suleiman	-	Jimbo la Wete
19	Mhe.	Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo

20.	Mhe.	Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
21.	Mhe.	Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
22.	Mhe.	Issa Haji Ussi (Gavu)	-	Jimbo la Chwaka
23.	Mhe.	Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
24	Mhe.	Juma Makungu Juma	-	Jimbo la Kijini
25.	Mhe.	Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
26	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	Jimbo la Donge
27.	Mhe.	Khamis Juma Mwalim	-	Jimbo la Pangawe
28.	Mhe.	Lulu Msham Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
29.	Mhe.	Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
30.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	Jimbo la Kiembesamaki
31.	Mhe.	Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
32.	Mhe.	Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
33	Mhe.	Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
34	Mhe.	Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
35.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Nafasi za Wanawake
36.	Mhe.	Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
37.	Mhe.	Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
38.	Mhe.	Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Jimbo la Mkoani
39.	Mhe.	Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
40.	Mhe.	Mohamed Ahmada Salum	-	Jimbo la Malindi
41.	Mhe.	Mohammed Said Mohammed	-	Jimbo la Mpendae
42.	Mhe.	Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
43.	Mhe.	Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini

44.	Mhe.	Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
45.	Mhe.	Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
46.	Mhe.	Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
47.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Jimbo la Chukwani
48.	Mhe.	Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
49.	Mhe.	Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
50.	Mhe.	Dkt Mwinyihaji Makame Mwadin i	-	Jimbo la Dimani
51.	Mhe.	Nadir Abdul-latif Yussuf	-	Jimbo la Chaani
52	Mhe.	Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
53.	Mhe.	Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
54.	Mhe.	Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
55.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	Jimbo la Amani
56.	Mhe.	Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
57.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	Nafasi za Wanawake
58.	Mhe.	Saada Ramadhan Mwenda	-	Nafasi za Wanawake
59.	Mhe.	Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
60.	Mhe.	Salama Aboud Talib	-	Nafasi za Wanawake
61.	Mhe.	Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
62.	Mhe.	Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
63.	Mhe.	Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
64.	Mhe.	Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
65.	Mhe.	Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
66.	Mhe.	Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
67.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Jimbo la Mgogoni

68.	Mhe.	Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
69.	Mhe.	Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
70.	Mhe.	Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
71.	Mhe.	Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
72.	Mhe.	Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
73.	Mhe.	Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
74.	Mhe.	Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
75.	Mhe.	Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
76.	Mhe.	Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
77.	Mhe.	Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

	Dkt. Yahya Khamis Hamad	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 4 Aprili, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

UCHAGUZI WA WAJUMBE WA TUME YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nitamuomba Katibu aeleze utaratibu wa uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, hiyo ndio shughuli yetu ya leo na Katibu ataielezea kutokana na Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Katibu.

Katibu: Mhe. Naibu Spika, leo tuko kwenye uchaguzi wa Wajumbe watatu wa Tume ya Bajeti chini ya kifungu 147(2), mnahitajika kuchagua wajumbe watatu ili waingie kwenye Tume ya Bajeti ya Baraza. Kuna orodha yenye wajumbe watano zitaletwa mbele yenu kuna alama ya ndio tu mbele ya huyo mgombea kati ya hao watano. Unachotakiwa u-*tick* watatu, hakuna ndio na hapana. Unatakiwa u-*tick* watatu ili watatu ambao watapata nafasi za juu hao ndio watakuwa wamechaguliwa na Baraza hili ikiwa ni Wajumbe wa Tume ya Bajeti, kati ya watatu hao itakuwa lazima awemo mmoja ambaye ni mwanamke. Kwa hivyo, watakaopata alama nyingi watatu wa kwanza hao ndio watakuwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, naona Waheshimiwa Wajumbe wanaangalia Kanuni. Kanuni ya 147(1) inatoa *composition,* inataja Wajumbe watano. Kanuni ya 147(2) inataja wajumbe watatu kwa hiyo kuna *confusion* lakini *practice* tunachagua wajumbe watatu. Mara zote hivyo ndivyo tunavyofanya na tumekubaliana na Mhe. Spika, kwamba turudie *practice* hiyo. Hata Baraza lililopita tulikuwa na wajumbe watatu kanuni ilikuwa hivyo hivyo na nilimjuilisha Mhe. Spika na Naibu Spika, na wakakubaliana kwamba tutumie hiyo *practice* ilivyo. Kwa hiyo, tutatoa *ballot* ya Wajumbe watano, tutachagua watatu kati ya hao watano.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kwa heshima na taadhima tugawe hizo *ballot* kwa ajili ya kufanya uchaguzi. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) naona ulikuwa una-*concern* hapo, lakini Katibu ameelezea vizuri labda utueleze *concern* yako hasa ni nini.

Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu): Mhe. Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi hii, hoja yangu ni kwamba nakubaliana na maelezo ya Katibu.

Ukisoma kifungu cha Kanuni 147(1), lakini ukisoma 147(2) kimeeleza vizuri kwa msingi wa kwamba kila chama cha siasa chenye uwakilishi katika Baraza kinaweza kupendekeza majina ya Wawakilishi. Sasa hoja yangu kwamba ukisoma kwa maudhui ya kila chama cha siasa nakubaliana na hiyo hoja ya kuchagua wajumbe watatu, lakini ukisoma kwa hoja ya wajumbe kwa mantiki ya wajumbe wa Kamati ya Bajeti naomba turudi kwenye namba ile ya tano tukiachana na huo msingi wa chama. Kwa sababu ukitizama hapa maudhui kana kwamba kuna vyama zaidi ya kimoja, lakini ukitizama namba yenyewe halisi ya wajumbe inatakiwa iwe watano. Sasa *unless* kwamba tunachukua watatu wengine tunaweka bakaa, sina hakika na huo uwakilishi wao uliokusudiwa hapa aidha wa majimbo, wa kuteuliwa ama kwa nafasi nyengine yoyote. Hapo ndipo palipokuwa na *confusion*.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwa busara zako hili jambo turudi kwenye kutizama maudhui ya Wajumbe wote kukamilisha namba na tuondokane na hii dhana ya uwakilishi kwa msingi wa vyama vya siasa.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Katibu.

Katibu Mezani (Ndugu Mussa Kombo Bakari): Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo tulitangulia kusema kuna *confusion* katika kanuni zetu, ipo dhana ya wajumbe watano na ipo dhana ya wajumbe watatu. Tumependekeza kwamba Wajumbe mridhie kuangalia mazoea ya Baraza lililopita. Kwa mfano, Waheshimiwa mkisoma kanuni ya 148(d) utaona inasema ifuatavyo naomba niinukuu Mhe. Naibu Spika:

Kanuni ya 148(d) inasema kwamba:

"Wagombea watatu watakaopata kura nyingi zaidi akiwemo mwanamke ndio watakaotangazwa kuwa washindi na kwamba wamechaguliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza".

Kwa hivyo, hiyo inaonesha moja kwa moja kwamba dhana inayopendekezwa na kanuni ni wajumbe watatu, sasa tukasema kwamba kumekuwa na mkanganyiko katika haya mambo na tukapendekeza kwamba wajumbe mridhie twende katika mazoea (*practice*).

Baraza lililopita wajumbe walikuwa ni watatu katika Tume ya Bajeti, alikuwemo marehemu Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Hija Hassan Hija. Hao ndio waliokuwa wajumbe wa Tume ya Bajeti waliochaguliwa na Baraza. Sasa hiyo ilikuwa ndio *practice*, tunaomba Waheshimiwa Wajumbe waridhie ili twende na *practice* kama ambavyo Mhe. Spika na Naibu Spika wamependekeza.

Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu): Mhe. Naibu Spika, naendelea kukushukuru kwa kunipa nafasi yako na sina dhamira labda ya kucheleweshe shughuli zilizopangwa na Baraza lako, lakini naomba tu kwamba nimesikiliza kwa makini sana hoja ya katibu mezani katika kifungu cha (d). Lakini naomba tu arudi katika kifungu 148(1) ambacho kimeeleza wazi kabisa suala la idadi na naomba tusijielekeze sana kwenye mazoea, inawezekana kwamba *precedent* nyengine ikawa sio nzuri na naomba tu turudi kwenye maelezo ambayo yameelezwa kwa uwazi na ufasaha kabisa katika kifungu 148 ambacho naomba nikinukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 148 kinasema kwamba:

"Utaratibu wa kuwachagua Wajumbe watano waliotajwa katika Kanuni ya 147(1)(g) utakuwa ni kama ifuatavyo:-

Umeendelea utaratibu na ninaamini kwamba majina matano tayari yameshapelekwa kwa Katibu kama vile ambavyo kifungu 148(a) kinavyojieleza. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri mumesikiliza hoja na wengine watakuwa tayari wameona katika Kanuni zetu zinasemaje kidogo zinakanganya. Sasa mimi nafikiria tufanye maamuzi kwa pamoja kwa maana ya kwamba nitatoa nafasi ya kupiga kura wale ambao wanasema waingie wajumbe watano basi wataingia wajumbe watano, lakini *ballot* yetu sasa tayari ina wajumbe watano hawa. Kwa hiyo sasa ikiamuliwa hivyo ina maana tutapumzika kidogo ili tubadilishe, tuongeze majina mengine kwa sababu hatuwezi tu kuchagua wakati wengine walikuwepo wameomba. Sijui mmenifahamu Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hiyo cha kufanya muhimu ni kwamba tunaweza tukaongeza majina mengine ili tupate *choice* ya kuchagua watu watano ambao tunawataka, sawa.

Kwa hiyo, naomba niwaulize Wajumbe wanaokubaliana na kuwa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi wawe watatu wanyooshe mikono, wale ambao wanasema wajumbe wawe watano wanyooshe mikono.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa kwamba idadi ya Wajumbe wa Tume ya Bajeti wawe watano)

Mhe. Naibu Spika: Kwa maana hiyo Waheshimiwa Wajumbe kwa pamoja mmekubali na mmetaka kwamba kutokana na Kanuni ya 147(g) ambacho kinaeleza wajumbe watano wasiokuwa mawaziri na manaibu mawaziri pamoja na Mwanasheria Mkuu watawaweza kuwa wajumbe wa Tume hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe kuna wazo hapa kwamba tayari tuna wajumbe watano ambao hawa ndio walioomba na walioletwa, sasa kama tutaendelea na *ballot* hii ya kusema wajumbe watano kuna uwezekano wa kuandika ndio au hapana, lakini kama tutaona kwamba tuongeze na wengine basi itakuwa kwa sababu hao wanakuja moja kwa moja kutoka kwa wanadhimu, makatibu wa chama. Kwa hiyo, nafikiria mimi tuendelee na uchaguzi tayari hawa walikuwa wameshachaguliwa watano tuendelee nao hivyo hivyo. Sasa *ballot* mtakayopewa ni hii ambayo inasema ndio au hapana lakini wajumbe watakuwa ni wale wale watano.

Katibu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa hiyo, *ballot* zetu sasa ambazo pia tumezitayarisha, kwa sababu tulitayarisha tukijua lolote linaweza kutokea tutatoa *ballot* za ndio na hapana ili mgombea awe amechaguliwa. Kwanza mtapigia watu watano kama tulivyosema ili mjumbe awe amechaguliwa na angalau apate nusu ya kura za Wajumbe, akikosa nusu ya kura za Wajumbe waliopo hapa huyo atakuwa hajachaguliwa, wanachaguliwa watano kwa ndio na hapana wote, kwa hiyo kila mmoja uta-*tick* ndio na hapana ni yule tu ambaye atapata hapana zaidi ya nusu ndiye atakuwa hajachaguliwa, lakini yeyote kati ya hawa ambaye atapata zaidi ya nusu ya kura za Wajumbe watakuwa wamechaguliwa kuwa ni wajumbe watano wa kuingia kwenye Tume ya Bajeti.

Waheshimiwa tunarudia, tunachagua wote watano tunachotaka ni ridhaa yenu kwa kila mmoja, kwa hiyo onesha alama ya ndio au hapana kwa kila mmoja, kila ambaye atakuwa amepata alama zaidi ya nusu ya kura za Wajumbe waliomo humu ndani ambao kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, tutawahesabu sasa hivi tuseme ni wangapi, baadae tutagawa *ballot* zetu tuanze kupiga kura. Nashukuru Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Naomba muanze kugawa karatasi.

Katibu: Mhe. Naibu Spika, wenzangu wananiambia ndani ya ukumbi kuna Waheshimiwa Wajumbe 72 na kwa ruhusa yako tunaomba tuanze kugawa *ballot* kwa ajili ya uchaguzi.

(Hapa Wajumbe walipiga kura)

Mhe. Naibu Spika: Naona mkono, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Kifungu 148(c) kinasema kwamba:

"Kila Mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Tume atapewa nafasi ya kujieleza kwa muda usiozidi dakika tano mbele ya wajumbe ndani ya Baraza kabla ya kupigiwa kura na wajumbe wanaweza kumuuliza mgombea huyo maswali yasiyozidi matatu".

Mhe. Naibu Spika, lakini utaratibu huo bado haujafanyika na kura zishagaiwa. Kwa hivyo, naomba utaratibu ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi nilifikiri kwamba tushakubaliana kuwa hao watano ndio ambao tutawachagua, kulikuwa hakuna *choice* nyengine ya wengine ambao wameletwa na nikatumia busara. Kwa hiyo, naomba mkubaliane na busara zangu.

Mheshimiwa sijakuruhusu usimame uzungumze, sasa nimekuruhusu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, nafikiri wazo lililotoka kwa Mjumbe mimi naliunga mkono. Kwa sababu ya msingi ni kwamba kuna wengine wanawatambua hao wajumbe na wengine hawawajui kabisa, ni vyema wakajieleza hata kama tukishapiga kura tukawaona sura zao japo wakae mbele kidogo tuwaone.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tumeshapiga kura, lengo na madhumuni ya kujieleza ni kwamba tunataka tujue tunayemchagua. Sasa tushapiga kura tusirudishe hii shughuli, Waheshimiwa tushapiga kura tuendelee.

Sawa, limetoka wazo kwamba wakati wa kuja kushukuru tutawaona na tutaweza kuwafahamu, ni vizuri kwa sababu hawa ndio makamishna wetu na hawa ndio watakaotuwakilisha katika Tume ya Bajeti ya Baraza, kwa hivyo ni vizuri sana kuweza kuwajua. Sasa nitawaomba wajumbe ambao wameomba nafasi hii wale watano waje kwa ajili ya kushukuru au watakuwepo hapo walipo na wataweza kushukuru baada ya matokeo.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe zoezi linalofuata itakuwa ni kwenda kuhesabu kura na ningeomba wale mawakala wa wagombea au wagombea wenyewe waseme ni nani ambao watakwenda kuwasimamia kura zao naomba asimame mmoja mmoja. Naomba Katibu unisaidie kutaja majina.

(Waheshimiwa wafuatao walitakiwa kutaja mawakala wa kusimamia kura zao)

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
3. Mhe. Rashid Ali Juma
4. Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma

(Waliotajwa hapo juu waliiamini meza)

5. Mhe. Lulu Msham Abdalla: Mimi nampeleka Mhe. Mihayo Juma N'hunga.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante naomba sasa maboksi ya *ballot* yachukuliwe. Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wamechagua mawakala naomba mawakala wao waende pamoja na maboksi na wengine tunashukuru kwamba wameamini meza. Katibu.

Katibu: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikupe taarifa kwamba wajumbe wawili wameongezeka wakati zoezi linaendelea. Kwa hiyo, wajumbe waliopiga kura ni 74 naomba kutoa hiyo taarifa, lakini baada ya hapo tunatakiwa kuahirisha kwa nusu saa.

(Hapa kura zilihesabiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kutokana na shughuli ya kuhesabu kura sasa tutaahirisha kikao chetu halafu tutarudi baada ya nusu saa.

(Saa 3:24 kikao kiliahirishwa kwa muda wa nusu saa
kwa ajili ya kuhesabu kura)

(Saa 04:00 asubuhi Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tukae. Katibu.

Katibu Mezani (Ndugu Mussa Kombo Bakari): Mhe. Naibu Spika, tunaomba kutoa taarifa kwamba zoezi la kuhesabu kura limekamilika. Hivyo, kwa idhini yako Mhe. Naibu Spika, naomba tusome matokeo kama ambavyo kura zilivyopigwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, Katibu alitoa taarifa kwamba wajumbe waliopo ndani ya Baraza ni 74, lakini wakati wa kuhesabu kura ni kwamba kura zilizokusanywa zilikuwa ni 73.

Sasa naomba nitaje matokeo kwa kila mjumbe mmoja mmoja na nikianza na Mhe. Hamza Hassan Juma, kura zilizomkubali zilikuwa ni 71, kura zilizomkataa ni 2 na hakuna kura iliyoharibika. *(Makofi)*

Kwa upande wa Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma, hakuna kura iliyoharibika, kura zilizomkataa ni 4 na kura zilizomkubali ni 69. *(Makofi)*

Mhe. Lulu Msham Abdalla hakuna kura iliyoharibika, kura iliyomkataa ni 1 na kura zilizomkubali ni 72. *(Makofi)*

Mjumbe mwengine ni Mhe. Rashid Ali Juma, hakuna kura iliyoharibika hata 1, kura zilizomkataa ni 2, na kura zilizomkubali ni 71.

Mjumbe mwengine ambaye ni wa mwisho katika orodha hii ni Mhe. Hamad Abdalla Rashid, hakuna kura iliyoharibika, kura zilizomkataa ni 3, kura zilizomkubali ni 70. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hayo ndiyo matokeo ya kura zilizopigwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii kuwapongeza sana wagombea wetu. Sasa naomba nitangaze kutokana na matokeo yaliyotolewa na Katibu, kwamba tayari rasmi wamechaguliwa na wamekuwa ni Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Hivyo, naomba niwataje tena wajumbe hao. Mwanzo ni Mhe. Hamza Hassan Juma, wa pili ni Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma, wa tatu Mhe. Lulu Msham Juma, wa nne Mhe. Rashid Ali Juma na wa tano ni Mhe. Hamad Abdalla Rashid. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe waliomba kwamba, wangetaka Waheshimiwa Wajumbe waliochaguliwa katika Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi wote watano, kila mmoja asimame kwa muda mdogo, kiasi kama dakika tano kwa ajili ya kuweza kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Naona mkono, Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, nafikiri kuna hitilafu ya jina Lulu Msham Abdalla, ameitwa Lulu Msham Juma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Mjumbe, ahsante. *(Makofi)*

Tunaanza na Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kutoa shukurani. Nianze kwako Mhe. Naibu Spika wewe mwenyewe kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuweza kuniamini na kunipa dhamana hii kubwa. Kwa kweli, dhamana hii ni kubwa kwa chombo chetu hichi, kwa sababu ni dhamana ambayo inayoshughulikia bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ndiyo inayotengeneza nyumba hii.

Kwa hiyo, naamini nitatumia uwezo pamoja na uzoefu wangu katika chombo hichi kwa kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanafanya kazi katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Pia nitajitahidi kusaidia kujenga hoja serikalini, ili kuhakikisha kwamba mambo ya Baraza la Wawakilishi yanakwenda bila ya mikwamo ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuweza kunipa ridhaa hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma, ahsante. Mhe. Mjumbe anayefuata ni Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma. *(Makofi)*

Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma: Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu la Wawakilishi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii ya leo kukutana na kuweza kufanya jukumu hili kwa salama na amani.

Pili, shukurani zangu za dhati kabisa nitoe kwa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote ambao wamenilitia kura za ndio, pamoja na wale waliotumia haki yao ya kidemokrasia kwa kusema hapana. Kwa kweli, wote ninawashukuru na ninawaambia ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kwa upande wangu, naomba niseme kama nilivyoanza kusema mwanzo na kila siku nikikutana na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ninawaambia, kwamba tukiangalia taswira ya Baraza hili, basi mimi ndiye kijana wenu mdogo kabisa kuliko wote kwenye Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, pamoja na udogo wangu huo hamkujali na mukasema kwamba kwenye kura hizi za ndio basi huyu kijana ndiye tunampa kura nyingi za kutosha za kuwa mjumbe halali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwenye hili ninawashukuru sana na tuko pamoja. Neno langu la mwisho nasema kwamba tutashirikiana na tutafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana, kijana wetu. Sasa tumpishe kijana mwengine Mhe. Lulu Msham Abdalla.

Mhe. Lulu Msham Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote walionichagua na wasionichagua na tutashirikiana kwa kuchukua maoni kutoka kwao na kuwasikiliza. Vile vile, kwa kuwatoa hofu hii kazi ninao uzoefu wa muda wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Lulu Msham Abdalla, ahsante sana. Sasa anayefuata ni Mhe. Rashid Ali Juma.

Mhe. Rashid Ali Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nichukue fursa hii awali kabisa kumshukuru *Allah Subhanahuu Wataalla* kwa kutupa afya njema na asubuhi hii kukutana tukiwa wazima sote.

Kwa kweli, sina mengi ya kusema. Mhe. Naibu Spika, na mimi nisirejee maneno na langu mimi ni kutoa shukurani. Hivyo, shukurani kama zilivyotolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote nakupeni shukurani zenu na ninaheshimu sana demokrasia iliyotolewa kwa wale waliotukataa na waliotukubali.

Kwa pamoja nataka niwaahidi kwamba, mumejenga Baraza jipya na hakika tutafanya kazi kwa pamoja na tutafikia malengo ambayo tumeyakusudia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Rashid Ali Juma, ahsante sana. mjumbe wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Hamad Abdalla Rashid karibu. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahuu Wataala*, kwa kuweza kutufikisha hapa leo tukiwa katika hali ya afya njema na kuweza kufikia malengo haya tuliyoyafanya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kutuamini. Hali hii imeonesha dhahiri kwamba wana imani na sisi. Mimi nisiseme mengi isipokuwa niseme kwamba tutashirikiana sisi Wajumbe wa Tume, Waheshimiwa Wajumbe wenzetu pamoja na watendaji wote wa Baraza, ili kuhakikisha kwamba Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi tunaifanya vizuri kwa kuzingatia hali ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wetu kwa kupiga kura za ndio na wale waliokataa na wala hawana maana ya kukataa, lakini walitimiza ile demokrasia yao katika uchaguzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, napenda kusema kwamba tutashirikiana na nyinyi bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunatimiza malengo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Katibu.

Katibu: Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo, tumemaliza shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Baraza lako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kutengua Kanuni, ili tuweze kumaliza shughuli hii ya leo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kazi zilizopangwa kwenye orodha ya shughuli za leo zimemalizika, naomba nitoe hoja ya kutenga kando Kanuni ya 23, ili tuahirishe kikao hiki hadi kesho siku ya Jumanne, saa 3:00 za asubuhi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu ya kutenga kanuni kando wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha kikao chetu hichi cha leo nina matangazo mawili. Kwa hiyo, naomba niyasome matangazo hayo. Tangazo la mwanzo Waheshimiwa Wajumbe wote munaombwa kubakia katika ukumbi huu kuna maelekezo muhimu ambayo yanatakiwa kutolewa.

Tangazo la pili, kuna wafanyakazi wa Bima ya Afya wamekuja wako juu kwenye makochi kwa ajili ya kuzungumza na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza. Kwa hivyo, wanaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza baada ya kumaliza hiyo shughuli ya hapa, basi wameshafika tayari na wala hatuwezi kusema kesho wakati watu wameshafika. Kwa maana hiyo, ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, tukimaliza shughuli ya hapa na wala haichukui muda, ni ndogo sana, basi tukimaliza twende juu kwa ajili ya kushughulikia mambo ya afya, kwani afya zetu ni muhimu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya matangazo haya niwashukuru sana kwa utulivu wenu pamoja na kuweza kutumia demokrasia ya kuchagua wajumbe wa Tume ya Bajeti, basi sasa kazi tunawaachia wao ili waweze kutuwakilisha vizuri ndani ya Tume hiyo.

Kwa hivyo, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 04:15 asubuhi kikao kiliahirishwa hadi
tarehe 05/04/2016 saa 3:00 asubuhi)